**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**Simu Na. +255 (026) 2963341/2963346**
**Nukushi: +255 (026) 2963348**
**Barua Pepe: ps@jamii.go.tz Tovuti: www.jamii.go.tz**

**Mji wa Serikali Mtumba Barabara ya Afya**
**S.L.P 573,**
**40478 DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAADHIMISHO YA WIKI YA USTAWI WA JAMII MWAKA 2025.**

**22, Agosti 2025 Dar Es Salaam**

Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau wa maendeleo imeandaa Maadhimisho ya Wiki ya Ustawi wa Jamii yenye lengo la kuimarisha na kuongeza ushiriki na uelewa wa wananchi kuhusu huduma za Ustawi wa Jamii, kuchochea uelewa mpana wa huduma hizi kwa jamii, kuhamasisha utetezi wa haki za kijamii na kuendeleza jamii jumuishi inayothamini usawa na ustawi wa makundi yote, hasa yale yaliyo katika mazingira hatarishi.

Kwa mwaka huu maadhimisho haya yanafanyika nchi nzima, ambapo Kitaifa yatafanyika Mkoani Dar es Salaam kuanzia tarehe 25 – 30 Agosti katika viwanja vya Chuo cha Ustawi wa Jamii Kijitonyama huku yakibeba hadhi ya kimataifa, yakileta pamoja washiriki kutoka nchi mbalimbali ikiwemo Kenya, Uganda, Zambia na Benin, yakiwa na kaulimbiu isemayo
***"Pata Msaada wa Kisaikolojia; Imarisha Afya ya Akili".*** Kaulimbiu hii inatoa wito kwa watu wote kuwa na ujasiri wa kutafuta msaada wa kitaalam wanapokumbwa na changamoto za kisaikolojia. Mgeni rasmi katika maadhimisho haya ni **Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Malengo ya maadhimisho haya ni: Kutoa elimu na kujenga uelewa kwa Umma kuhusu huduma za Ustawi wa Jamii zinazopatikana nchini; Kuchochea matumizi na maboresho ya Sera, Sheria na Miongozo ya huduma za Ustawi wa Jamii; Kuhamasisha na kuimarisha ushirikiano kati ya Wadau wa huduma za Ustawi wa Jamii; Kubadilishana uzoefu katika utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii kutoka nchi nyingine; Kuwezesha Maafisa Ustawi wa Jamii kuboresha utoaji wa huduma; na Kuhimiza Ulinzi na Usalama wa makundi maalum katika jamii ikiwemo Wazee, Watoto na Watu Wenye Ulemavu.

Maadhimisho haya yataambatana na utoaji wa huduma ya ustawi wa familia na watoto; elimu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu; huduma za marekebisho, ujenzi wa tabia na haki za mtoto kisheria, msaada wa


kisaikolojia na kijamii, ushauri na unasihi, elimu ya malezi chanya na ulinzi na usalama wa mtoto, usajili wa vituo vya kulelea watoto wachanga na wadogo mchana, Huduma ya Afya ya Akili, Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii, usajili wa Makao ya Watoto na Nyumba Salama, Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa na familia, elimu kuhusu Malezi ya Kambo na Kuasili, Haki za Mtoto Kisheria na huduma kwa makundi maalum ikiwemo Wazee na Watu Wenye Ulemavu.

Pia katika Wiki ya Ustawi wa Jamii zitatolewa huduma za upimaji wa afya kwa Wazee; huduma za kibingwa na bobezi; huduma kwa manusura wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya Watoto; huduma za msaada wa kisheria, huduma ya rufaa na maonesho ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana.

Napenda kutoa wito kwa Watanzania wote, kujitokeza kwa wingi kushiriki katika maadhimisho haya, ili kunufaika na huduma na elimu mbalimbali zitatolewa bure katika mabanda ya maonesho kwenye viwanja vya Chuo cha Taasisi ya Ustawi wa Jamii kilichopo Kijitonyama Mkoani Dar es Salaam. Pia, huduma kama hizi zitatolewa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini.

Maadhimisho haya yameambatana na shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na; Kufanya kampeni ya utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii katika halmashauri 184 nchini, Utoaji elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu huduma za Ustawi wa Jamii na upatikanaji wake nchini; maonesho na utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii unaohusisha sekta mbalimbali ikiwemo afya na msaada wa kisheria, maonesho na kongamano la wamiliki wa Makao ya Watoto, Nyumba Salama na Vituo vya kulelea watoto wachanga na wadogo mchana na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Maafisa Ustawi wa Jamii nchini utakaojumuisha maafisa ustawi kutoka nchi za nje.

Katika kuijenga Tanzania jumuishi, yenye usawa, mshikamano, na inayothamini utu wa kila mmoja Wiki hii ni muhimu kwa ustawi wa jamii kwa ujumla. Tujitokeze kwa wingi kushiriki shughuli mbalimbali katika Wiki hiyo na kwenye kilele chake tarehe 30 Agosti, 2025 kwa mustakabali wa ustawi wetu.



Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**